

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**  
**MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA**  
**TAREHE 11/02/2016**

**MAHUDHURIO,**

1. MH. ERICK E. NKILAMACHUMU	MWENYEKITI
2. BW. KEVIN S. MAKONDA	KATIBU(DED)
3. MH.JOHN M. SHIMI I'MANA	MJUMBE
4. MH.MKUBILA S. SOUD	MJUMBE
5. MH.ADRONIZI E. BURINDOLI	MJUMBE
6. MH.OLIPA A. BUGOKE	MJUMBE
7. MH.KHAMIS B. HAMADI	MJUMBE
8. MH.ROMAN MITABARO	MJUMBE
9. MH.JUSTUS K. MASUMO	MJUMBE
10. MH.DAVID I BUZUTU	MJUMBE
11. MH.GWIHANGWE M. EDWARD	MJUMBE
12. MH. VAILETH MADENDE	MJUMBE
13. MH.SAID R. SOUD	MJUMBE
14. MH.ZAWADIA. COSMAS	MJUMBE
15. MH.WILBARD J.BAMBARA	MJUMBE
16. MH.GWASSA NTUNGIYE	MJUMBE
17. MH. SUZANA BAHATI	MJUMBE
18. MH. FIDEL F. NDANGWA	MJUMBE
19. MH.MUKIZA S. BYAMUNGU	MJUMBE
20. MH.NZEYE LEONARD	MJUMBE
21. MH.SENTORE J. MIBURO	MJUMBE
22. MH.PHILBERT M KIIZA	MJUMBE
23. MH.MATHIAS E. MUGATA	MJUMBE
24. MH.GEORGIA MUNYONYELA	MJUMBE
25. MH.KAGOMBA S. GEORGE	MJUMBE
26. MH.LAURENT J. MUSUNGARERE	MJUMBE
27. MH. JOHN E. RUZIGE	MJUMBE
28. MH.CATHERINE EDWARD	MJUMBE
29. MH.REHEMA S. RAMADHANI	MJUMBE
30. MH.SAFARI M. BANIGWA	MJUMBE
31. MH. EDITHA MWINULA	MJUMBE
32. MH ALEX GASHAZA(MB)	MJUMBE

**WAJUMBE WAALIKWA**

1. BW. SMITH SWAI	MWANDISHI WA HABARI, RK
2. BW. HUDSON BAGEGE	MWENYEKITI- CCM(W)
3. BW. JACOB MAKUNE	KATIBU- CCM (W)

**WATAALAM WALIOHUDHURIA:**

- |   |                            |
|---|----------------------------|
| 1. BW. BIGAMBO AMOS                     | AFISA MIPANGO (W)          |
| 2. BW. MASOUD ABDALLAH                  | MWEKA HAZINA               |
| 3. BW. WILFRED MAGIGE                   | MKAGUZI WA SHULE(W)        |
| 4. BW. ADELINA MAPUNDA<br>BIASHARA(W)   | KAIMU AFISA                |
| 5. BW. GASPAR BALTAZAR                  | AFISA USAFIRISHAJI WA HW   |
| 6. BW. BULILO MUSOMBWA DEYA             | MWANASHERIA WA (W)         |
| 7. BW. RUKIZA ABEID                     | AFISA TEHAMA               |
| 8. BW. F.M KAPAMA                       | MKAGUZI WA NDANI           |
| 9. BW. GRATION LAUREAN                  | KAIMU MUHANDISI WA MAJI    |
| 10. ENG. SIMEON W. NDYAMUKAMA           | MHANDISI (MAJI)            |
| 11. BW. JULIUS ERNEST<br>NYAMIHAGA      | KNY AFISA TARAF            |
| 12. BW. THEONEST THADEO                 | KAIMU AFISA TARAF KANAZI   |
| 13. BW. MORIS MOMBIA                    | KAIMU AFISA TARAF RULENGE  |
| 14. BW. PASTORY M. MSABILA              | AFSA TARAF MURUSAGAMBA     |
| 15. BW. CONSTANTINE MUDENDE<br>WILAYA   | KAIMU AFISA KILIMO         |
| 16. BW. FIDELIS MALIMBU<br>SEKONDARI(W) | K/AFISA ELIMU              |
| 17. BW. SANGATATI JOSEPHAT              | K/AFISA MIFUGO NA UVUVI(W) |
| 18. BI. SAKINA CHAMITI                  | MRATIBU WA TASAF           |
| 19. BW. JOSEPHINE LUSATILA<br>JAMII(W)  | K/AFISA MAENDELEO YA       |
| 20. BI. PERPETUA RULIMBIYE              | AFISA UGAVI (W)            |
| 21. BW. CHARLES C. MBEIKYA<br>MSINGI(W) | K/ AFISAEIMU YA            |
| 22. BI. BETTY S. MUNUO                  | AFISA ARDHI(W)             |
| 23. BW. TOBA MUHINA                     | AFISA MAZINGIRA(W)         |
| 24. DR.NELSON RUFANO                    | KAIMU MGANGA MKUU(W)       |
| 25. BW. PHILIP ILETA                    | AFISA MISITU (W)           |
| 26. BW. OWDEN MBUBA                     | AFISA UTUMISHI(W)          |
| 27. BW. MICHAEL NDYAMUKAMA              | KATIBU TSD(W)              |
| 28. BI. MWAJUMA M. NGOMUO               | AFISA ARIDHI               |
| 29. BW. SABUNI S. KASUBI                | MUHANDISI UJENZI           |
| 30. BW. REINFRIDA ANZIGARY              | MRATIBU WA VIKAO(W)        |

### **MUHT NA 12/2015/2016: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwasalimia wajumbe na kuwaeleza wajumbe kuwa walipata mgeni na kuwaomba wajumbe kukaribisha na kumsikiliza. Kikao kilifunguliwa saa 5.20 asubuhi

### **MUHT NA 13/2015/2016: KURIDHIA AGENDA**

Wajumbe walijadili na kupokea agenda.

### **MUHT NA 14/2015/2016: TAARIFA ZA KATA KATA YA BUKIRIRO**

Taarifa iliwasilishwa kama ifuatavyo; Kata ya Bukiriro ina vijiji 4 Kaya 5075 wanancode 588 na wanawake 122 kgografia imepaka na Kata ya Rulenge, Bugarama, Kibogora na Kata ya Mbuba, ilishafanya vikao vya ulinzi na usalama kwa 100% vikao vya VDCvilifanyika 2 kimoja hakijafanyika, miradi yamaendeleo iliyoko katika Kata ya Bukiriro ni ujenzi wa nyumba za waalimu, Kata ya Bukiriro haipo katika mradi wa kunusuru kaya maskini TASAF, mradi huu upo katika kijiji cha Mumuhamba, shule zipo 7, bado kuna mahitaji ya waalimu wa shule za msingi, vyoo, madawati madarasa na jengo la utawala, shule zote za msingi zimepata fedha za ruzuku Tshs.1,526,843.33 na matumizi yaliyofanyika ni Tshs. 1,456,000/=

Pia Kuna kituo cha Afya

### **KATA YA RUSUMO**

Kata ya Rusumo ina vijiji 3 na vitongoji k13 ina kaya 3078 na idadi ya wakazi 12,312, ina shule za sekondari 2 moja ya serikali na nyingine binafsi, ina zahanati 2 na shule za msingi 4,kuna changamoto ya ukosefu wa maji, wakazi wanaopata maji ni 65% na wasipata maji ni 34%, ina wagonjwa wenye VVU wapato 32 amba walijikubali sawa na 0.001%, hali ya ulinzi na uusalama ni nzuri

### **KATA YA MURUSAGAMBA**

Kwa upande wa mashariki inapaka na Wilaya ya Biharamulo, Magharibi inapakana na Kata ya Muganza na kaskazini kata ya Nyamagoma kusini inapakana na Mkoa wa Kigoma, ina jumla ya vijiji 3 na vitongoji 21, kuna kaya 2470 na wakazi wapatao 15547 ambapo wanaume ni 6003 na wanawake 9544,wakazi wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya chakula na biashara, vikao vya kisheria vilifanyika kwa 100%, ina shule za msingi na sekondari na soko la murusagamba, pia kuna zahanati 1.

### **KATA YA NTOBYEYE**

Kata ya Ntobeye katika kipindi cha robo ya pili shughuli za maendeleo zilisimamiwa na Kamati ya maendeleo ya Kata(WDC) bila diwani, vikao vya WDC vilivyofanyika ni 3, wananchi wamechangia katika ujenzi wa miundombinu kama vile maabara katika shule ya sekondari Ntobeye, masomo ya elimu ya msingi yanaendelea vizuri kwenye shule 5, kuna zahanati ya Ntobeye, hali ya kilimo ni nzuri hasa katika kilimo cha viazi vitamu, viazi

mviringo, nyanya, karoti n.k, zoezi la kutokomeza mnyauko linaendelea kuna miradi mingine inayoendelea kama vile mradi wa TASAF III

### **KATA YA KIBIMBA**

Kata ya Kibimba inaundwa na vijiji 4 na vitongoji 20, kunakaya 2732 zenye wakazi 15071 ambapo wanaume ni 6861 na wanawake ni 7710, ina shule za msingi 5, chuo cha ufundi cha shirika la REDESO, zahanati 4, uwanja wa ndege wa kimataifa Ruganzo, kata inatoo huduma ya umeme na maji, hali ya ulinzi na usalama ni nzuri, ina viongizi wa ngazi mbalimbali, na watumishi wa umma

### **KATA YA MABAWE**

Taarifa iliwasilishwa kama ifuatavyo, Kata ya mabawe ni mionganini mwa kata 5 zilizopo katika Tarafa ya kanazi, upandewa kaskazini magharibi inapakanana Burundi na upande wa ndani ya nchi inapaka na Kata ya Mugoma, Kanazi na Kata ya Kabanga, ina vijiji 5, ina viongozi wa kuchaguliwa, ina wakazi 12,440 wanaume ni 5915 na wanawake 6525, ina sekta ya elimu, afya maji, kilimo, mifugo, ujenzi, utawala na maendeleo ya jamii, mazingira, na ardhi. Suala la ulinzi na usalama linaendelea kuimarishwa, vikao vya kisheria vilifanyika kwa 100%.

### **KATA YA NYAKISASA**

Taarifa iliwasilishwa kama ifuatavyo, Kata ya Nyakisasa ni mionganini mwa Kata zilizoko katika Tarafa ya Rulenge, imeundwana vijiji 4 na vitongoji 19, ina idadi ya Kaya 5027, idadi ya watu 23235, wanaume 11266 na wanawake 11969, Kata ina watumishi waliopo katika ngazi ya utawala na walaamu pamoja na viongozi wa vijiji, Taasisi zilizopo Kata ni shule ya sekondari, zahanati 3, mahakama 1 haifanyi kazi, madhehebu ya dini 6, ofisi ya kata, kijiji, mek, Afisa kilimo na ofisi ya diwani. Vikao vya kisheria zilifanyika kwa asilimia 100% WDC vikao 4, VDC vikao 12.

### **KATA YA BUGARAMA**

Inaundwa na vijiji 3, na vitongoji 13, ina kaya 3348, na wakazi wakazi wapatao 14,214, inapakanana Kata ya Bukiriro na Kata ya Muganza, ina viongozi wa Serikali, kuna shule zahanati na wakazi wanajishughulisha na kilimo, vikao havikufanyika kwa 100% kwa sababu ya ukosefu wa mahudhurio ya wajumbe na ukosefu wa vitendea kazi, vyanzo vya mapato vilikuwa chini ya mawakala kwa kipindi cha mwezi 10-12 2015

### **KATA YA KANAZI**

Kata ya ipo karibu na makao makuu ya Wilaya ya Ngara, ina shule za msingi, pamoja na shule ya sekondari, kuna kituo cha Afya 1, kata inatoo huduma ya umeme na maji, hali ya ulinzi na usalama ni nzuri, ina viongizi wa ngazi mbalimbali, na watumishi wa umm. Kuna Mahakama ya mwanzo 1 na kituo kidogo cha polisi 1, kuna soko linalofanyika kila siku ya jumanne, pia wakazi wanajishughulisha na kilimo pamoja na ufugaji

### **KATA YA KIBOGORA**

Inapakanana Tarafa ya Rulenge, ina vijiji 2, ina jumla ya Kaya 3434 wakazi 14870 ambapo wanaume ni 6435, na wanawake 8435, ina vitongoji 9, ina viongozi wa kuchaguliwa, vikao vya kisheria vinafanyika kwa 100%, ina Baraza la Kata 1, hali ya ulinzi na usalama ni nzuri, maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi yapo kwa kiwango kidogo, kuna shule ya sekondari

kibogora, zahanati 2, wakazi wanajishughulisha na kilimo pamoja na ufugaji.

### **KATA YA MUGOMA**

Kata ya Mugoma inapakana na Kata ya Kanazi, kwa upande wa mashariki na upande wa kaskazini Kata ya Ntobeye magharibi inapaka nan chi jirani ya Burundi. Ina wakazi 15048, wanaume 7392 na wanawake 7656, ina vijiji 5, ina viongozi wa kuchaguliwa na watumishi wa umma, huduma za ukimwi zinatolewa au kuratibiwa na shirika la Tumaini Fund, ina jumla ya vitongoji 22 na kaya 2882, ina shule za msingi 5, shule za sekondari 2, Mahakama ya mwanzo 1, zahanati 3, vituo vidogo vya polisi 2 na madhehebu mbalimbali ya dini, wakazi wanajishughulisha na kilimo, ufugaji na biashara, vikao vya kisheria vilifanyika kwa 100%

### **KATA YA NGARA MJINI**

Kata ya Ngaramjini ipo ndani ya mamlaka ya mji mdogo Ngara ina jumla ya vijiji/mitaa 4 yenye vitongoji 17 viongozi wa kuchaguliwa wapo 17 na 7 viti maalumu, kikao kilichofanyika katika kata ya Ngara Mjini ni kimoja ambacho cha ulinzi na usalama vikao vingine viro kwa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji mdogo Ngara, kuna Baraza la Kata 1 ambalo ni baraza la Kata la ardhi, vyanzo vya mapato ni ushuru wa masoko, mazao, ndizi. Maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi kwa sasa yamepungua kutoka 1.1% hadi 1%

### **KATA YA MURUKULAZO**

Kata hii inapakana na Kata 3 na nchi jirani ya Rwanda, upande wa kusini inapaka na Nyamiaga, na upande wa kusini inapakana na Rusumo, na upande wa magharibi inapaka na Kata ya Ntobeye, inaundwa na vijiji 5 na vitongoji 26, kuna vyanzo vya mapato kuna soko la Murunyinya na ushuru wa nyama.

### **KATA YA RULENGE**

Ni mionganoni mwa Kata 2 zilizopewa hadhi ya kuwa mamlaka ya mji mdogo ndani ya Wilaya ya Ngara, ina wakazi 17,313, ina kaya 3950, kati ya hao wanaume 8252 na wanaume 9061, ina sekta Elimu, mifugo, uvuvina ushirika, ulinzi na usalama pamoja na ukusanyaji wa mapato, ina viongozi wa ngazi mbalimbali, kuna baraza la Kata.

### **KATA YA KEZA**

Kata inaundwa na vijiji 2 ambavyo ni kazingati na keza, ina idadi ya kaya 2162, wanaume 4034 na wanawake 4910, shughuli za kiuchumi wakazi wa Kata ya keza wanalima mazao ya chakula na biasharana ufugaji pia, ina shule 4 na zahanati 2, vikao vya kisheria vilifanyika kwa asilimia 100.

### **KATA YA NYAMAGOMA**

Kata ya Nyamagoma inapakana na Wilaya ya Biharamulo, Kankoko, Kata ya keza, Murusagamba, na Muganza, inaundwa na vijiji 3 na vitongoji 13 ina kaya 1242, ambapo ina jumla ya wakazi 7281 kati yao wanaume ni 3424, na wanawake 3857, vikao vya kisheria vilifanyika kwa 100% ina shule za msingi na sekondari, wakazi wanajishughulisha na kilimo na vyanzo vya mapato vinatokana na ushuru wa mazao.

### **KATA YA MBUBA**

Kata inaundwa na vijiji 4, na vitongoji 16, kaya 2586 na wakazi 13702, wakazi wa Kata ya

Mbuba wanajishughulisha na kilimo na ufugaji, ina shule za msingi 4 na shule za sekondari 2, hali ya ulinzi na usalama ni nzuri.

### **KATA YA KIRUSHYA**

Inapakana na Kata ya Mugoma na Ntobeye, nchi jirani ya Burundi na upande magharibi imepakana na mto Kagera na upande wa kaskazini nchi ya Rwanda, na kwa upande wa magharibi, ina vijiji 4, idadai ya wakazi 12804 kati yao wanaume ni 5552 na wanawake 7252, ina viongozi wa kuchaguliwa na watumishi wa umma, vikao vilifanyikawa 100%, kuna Baraza la Kata na vyanzo vya mapato ni ushuru wa vibanda, kahawa na mazao. Kuna shule ya sekondari kirushya na hali ya usalama ni nzuri isipokuwa kuna changamoto ya wakimbizi wanaokuja kuomba hifadhi toka nchi ya Burundi.

### **KATA YA KASULO**

Inaundwa na vijiji 3, ina jumla ya Kaya 3731, idadai ya watu 17032, ambapo wanaume ni 8424 na wanawake 8608, vikao vya kisheria vilifanyika, hali ya ulinzi na usalama ni shwari, hali ya kiuchumi wakazi wanafanya biashara za jumla na rejareja, hotel na migahawa, minada ya ng'ombe, baa na nyumba za kulala wageni, josh, kilimo cha mazao na ufugaji. Ina shule za msingi 7, Sekondari 2, Zahanati 2, Kituo cha Afya 1, kituo cha polisi 1, Mahakama ya mwanzo 1, Masoko 3 maji ya bubujiko na barabara kuu za mitaa

### **KATA YA KABANGA**

Kata ya Kabanga iko umbali wa Km 26 kutoka makao makuu ya Wilaya ya Ngara, inapaka na Kata ya Mabawe na Kata ya Mbuba, aidha upande wa magharibi inapaka na nchi jirani ya Burundi. Ina jumla ya kaya 4366 zenye jumla ya wakazi 23543 ambapo wanaume ni 10,763 na wanawake 12780, ina vijiji 6 na vitongoji 25, ina shule za msingi 7 na shule za sekondari 2, kuna zahanati 3, wakazi wa Kabanga ni wakulima pia ni wafugaji, vikao vya kisheria vilifanyika kwa asilimia 100, ina misikiti 4 na makanisa 28 ipo minara ya simu ya TTCL na VODACOM

### **KATA YA NYAMIAGA**

Kataya Nyamiaga ina vijiji 2 Nyamiaga na Nterugwe, vikao vya kisheria vilifanyika kwa 100%, ina jumla ya kaya 1522, jumla ya wakazi 11010, wanaume 5023 na wanawake 5637, hali ya ulinzi na usalama ni nzuri, wakazi wanajishughulisha na kilimo, ufugaji na biashara, ina shule za msingi 3, zahanati 1 baraza la kata, huduma ya umeme na maji barabara, makanisa 12 misikiti 2 na vikundi vya vikoba na saccoss.

### **KATA YA MUGANZA**

Kata hii iko kusini mashariki mwa Wilaya ya Ngara, ina jumla ya wakazi 156161 ambapo wanawake ni 8061 na wanaume 7555 na jumla ya kaya 3528. Ina jumla ya vitongoji 19, ina viongozi wa kuchaguliwa na watumishi wa umma, wakazi wa Kata ya Muganza wanajishughulisha na kilimo na ufugaji, Kata ina shule 8 za msingi na shule ya sekondari, vyanzo vya mapato ni masoko ya Mkubu na Mukaliza, vikao vya kisheria vinafanyika

**MUHT NA 15/2015/2016: MAPENDEKEZO YA BAJETI KWA MWAKA 2016/2017**

Katibu alisema kwamba mapendekezo haya yametokana na mapendekezo yaliyotolewa katika kamati za huduma za jamii na kamati ya uchumi, ujenzi na mazingira wamejaribu kuanisha ,mapendekezo yote katika kuboresha bajeti yetu, na kumuomba Afisa Mipango awasilishé mapendekezo ya bajeti kwa mwaka 2016/2017

Masahihisho kwenye bei ya mazao ya ndizi kutoka 300-500

Mjumbe alisema kuwa aliongelea kuhusu shule ya msingi ya Nyamahwa, Mukibogoye na Katerere anaomba na shule ya msingi Nyamiaga yenyé madarasa yanayotaka kuanguka iwekwe kwenye bajeti hii au kwemye bajeti ya 2017/2018, Upimaji wa miji midogo bajeti hii pia iweke mji wa Ngara mdogo

Mjumbe alisema kuwa anazungumzia katika kamati ya elimu, shule ya msingi kigoyi ipo kwenye bajeti, zahanati ya Kumugamba sio ujenzi ni ukarabati

Mjumbe alisema kwamba alifikiri kwenye bajeti hii marekebisho yafanyike katika elimu ya msingi, kwenye kamati ya fedha ilizungumzwa masuala ya vyoo katika shule msingi, shule ya msingi Kagali ina vyumba 2, lakini kwenye bajeti hii hakuna mpango wa kuongeza vyumba katika shule hii.

Aidha mjumbe alisema kwamba Mradi wa Nterugwe ni kero sana na ni mradi wa siku nyingi, ingetakiwa umalizike katika miradi viporo au wahusika watuambiwe watafanya nini.

Ukurasa namba 5, kwenye magari wanayobeba mzigo mkubwa anafikiri watozwe faini

Uk. 3 katika kuimarisha utunzaji wa mazao aliiomba idara husika isaidie kutoa mifuko ya kuhifadhia mazao.

Aliongeza kuwa Kijiji cha Minara hakina Zahanati watu wanaenda kupata huduma katika zahanati ya Kihinga hivyo suala hili liangaliwe kwa makini, na hajjawekwa kwenye bajeti ya 2016/2017 na 2017/2018, Rwinyana hajjawekwa kwenye mradi wa maji.

Afisa Elimu Msingi alisema kwa upande wa shule ya nyamiaga wamelipokea, shule ya msingi Burengo wananchi walikuwa hawajakubaliana na waraka wa elimu bure namba 6, badaa ya kujadiliana kwa kina walikubaliana watoe Tshs. 5000/= na TCRS walikubali kutoa vifaa vya ujenzi, walishauri kama uwezekano upo watengeneze vyumba vya madarasa vya muda, kwa kifupi bajeti imezingatia kuwa miradi viporo yote itekelezwe na hakuna miradi mipyä, Wiki hii wametuma taarifa TAMISEMI kueleza au kutoa tathimini ya mahitaji ya shule na taarifa hii tayari imeshafika TAMISEMI.

Mwenyekiti alisema itafutwe namna yoyote matatizo yaliyopo katika kila shule baada ya wanafunzi wengi kuripoti baada ya kutolewa Waraka wa elimu bure bila malipo, pia tutafute mafundi vijiji wajenge hata mashimo 2 ya vyoo.

Aidha alisema kwamba Kuhusu fundi, shimo la choo kama litakuwa tayari TCRS wapo tayari kutoa vifaa vya kiwandani wananchi hawajalazimishwa wachangie hela ya fundi, idara ya elimu haijapokea fedha na kwa sababu taarifa zimetumwa tamisemi fedha itakapoletwa shule hiyo itapewa kipaumbele.

**AZIMIO:** kikao cha kamati ya fedha itafutwe Tshs. 2,000,000/= tupeleke fedha katika shule ya Burengo na hatuwezi kufunga shule

Mwenyekiti alisema pia kwamba mahitaji yamekuwa makubwa katika shule zetu kwa sababu ya waraka wa Elimu bure, Idara ya Elimu iangalie pia katika shule ya Mukibungeye

Mhandisi wa maji alisema mradi wa maji Nterungwe haujaonekana katika bajeti kutockana na ukomo wa bajeti, kwa muda mrefu fedha za OC hazijaletwa, fedha zitakapopatikana mradi huu utapewa kipaumbele, na kama OC haitaletwa aliomba kuipoleka katika bajeti ya mwaka unaofuata, pia mradi wa Rwinyana

Mwenyekiti alisema kuwa mradi wa Mujebwe umefika 60%, lakini wa Rwinyana upo kwa asilia 90%, alimuomba Muhandisi awasiliiane na Mkandarasi walau afungue maji japo anatudai.

Afisa Kilimo alisema kuwa mifuko ya kutunzia mazao ina mifuko 2 mmoja upo kwa nje na mwingine kwa ndani ikifungwa vizuri wadudu hawawezi na kuingia kuharibu ila kama Idara haina uwezo wa kugharamia mifuko ila waliwaomba wananchi wanaohitaji waende pale stendi duka la ikoma na caritas rulenge.

Mjumbe aliomba Maafisa Ugani wazunguke na kutoa elimu juu ya kuhifadhi mazao, na ile sampo ya gunia lililofungwa ibaki kijiji.

Afisa kilimo alijibu kwamba Wagani walioko katika maeneo yetu walizunguka na kutoa elimu, na wanaamini walifanikiwa.

Mwenyekiti alisema aliwaomba Maafisa ugani watoe elimu mazao yanahifadhiwa kwa muda gani katika mifuko hiyo.

Mhandisi wa Ujenzi alisema kuwa anaamini madereva wanafahamu alama za barabarani, ila kwa atakayekiuka atatozwa faini, atawasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Kahama kuona wanatoza faini kiasi gani.

Afisa Ardhi alisema bajeti ya kupima viwanja mjini mipango miji ipo na Halmashauri haijalipa fidia kwa watu na bado wameshikilia viwanja vyao, Halmashauri itenye fedha kwa ajili ya kulipa fidia, kwenye bajeti wameweka bajeti ya kuweka mipango miji na bajeti nyingine itawekwa kwa ajili ya kufanya uthamini na maeneo yatamilikisha kwa Halmashauri.

Mwenyekiti alisema alimuomba Afisa Ardhi aweke bajeti ya kupima maeneo yetu ya Ngara Mjini kwa sababu hapa tulipo bado hayajapimwa

Afisa Ardhi alisema kuwa eneo lazima liwe na eneo la mipango miji na hawezi kupimiwa mtu mmoja kwa sababu maeneo mengi pia, ili kutambua hapa kuna shule au barabara.

Mjumbe mmoja alisema majibu ya Afisa Ardhi hayana msaada kwa sababu walitegemea kwenye bajeti kama hii Idara ya Ardhi ingetenga bajeti ya kupima katika maeneo kadhaa, waliomba waanishe maeneo , wataalamu waje na mpango wa upimaji uendelee.

**AZIMIO:** Mapendekezo yatajadiliwa kwenye CMT na kuletwa katika kikao kijacho na hili pia ni Agizo la serikali kupata hati miliki katika viwanja vyake

Mradi wa maji ambao wananchi walichimba mtaro kwa muda mrefu ingawa fedha zake hazijaletwa anaomba Mhandisi wa Maji ajaribu kuangalia katika Oc itakayoletwa au iwekwe kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018

#### **MUHT NA 16/2015/2016: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA**

Wajumbe walifanya masahihisho yafuatayo;

*Jina la John Shimiimana isomeke -John Shim'iman*

*Edward M. Gwihangwe lisomeke -Gwihangwe M. Edward*

*Ruzige Eliazary lisomeke -John J. Eliazary*

*Burindori lisomeke -Burindoli*

*Kaliyo Justus Masumo lisomeke -Justus Kaliyo Masumo*

#### **MUHT NA 17/2015/2016: TAARIFA ZA UTAWALA**

Afisa Utumishi aliwasilisha taarifa. Mwenyekiti waliwakaribisha wagombea kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira waweze kujitambulisha na baadae kutoa wasifu wao. Jumla ya wagombea walikuwa 4, Bw. George Rubagora,Bw. Jonam Rukanda, Bw. Charles Mushatsi na Bw. Felix Nyilema.

Baada ya kutoa wasifu wao Mjumbe mmoja alimuuliza Bw. Felix Nyilema kuwa kama amesomea sheria za kazi, je sheria hiyo ilianza kutumika Lini?, Alijibiwa kwamba sheria hiyo ilianza kutumika mwaka 2003

Mjumbe alimuuliza Bw. Charles Mushatsi kwamba nafasi hii inamtaka mtu mwenye sifa ya uelewa wa masuala ya sheria, na Utawala, ye ye ni Mtabibu je kwa nafasi hii atawezajje kufanya kazi, Alijibiwa kuwa Mwenyekiti sio lazima awe na taaluma zilizotajwa kwenye tangazo la kazi kwa sababu kutakuwa na Wataalamu kazi yake ye ye itakuwa ni kuwasimamia.

Ulifuata Utaratibu wa kupiga kura, wajumbe 27 walipiga kura baada ya zoezi hilo matokeo yalikuwa kama ifuatavyo;

Bw. Charles Mushatsi alipata kura 2

Bw. Jonam Rukanda alipata kura 5

Bw. Felix Nyilema alipata kura 9

Bw. George Rubagora alipata kura 11

Baada ya kutolewa kwa matokeo Bw George Rubagora aliibuka mshindi kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira.

Wagombea waliwashukuru wajumbe kwa kuwapigia kura, Bw. George Rubagora aliwashukuru kwa kupata nafasi na kuibuka mshindi alihaidi kuwa mwaminifu na mwadilifu na anaamini anafaa katika nafasi hiyo, alishawahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya shule 3 za Sekondari, Mwenyekiti wa huduma za uchumi kwa miaka 14, na Mwenyekiti wa huduma za jamii kwa miaka 10,Mwenyekiti wa Bodi ya Afya na kusema kama Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira kazi yake ni kusimamia, kuelekeza, kuongoza na kushauri.

Mjumbe mmoja alitaka kufahamu kuhusu taarifa ya Lumasi ambayo ilitakiwa kuletwa kwenye kikao

Mwenyekiti alisema kuwa kwa sababu ni suala la kiutumishi na jambo hili linatakiwa lifanyike kushirikiana na wajumbe wengine toka Mkoani.

Mjumbe mwengine alisema kwamba kitiishwe kikao maalumukujadili taarifa ya Lumasi

Mjumbe mmoja alisema kwamba kwa sababu kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kitafanyika tarehe 18/03/2016 siku hiyo ya kikao ndipo tarehe ya kikao cha Baraza la Madiwani itapangwa. Wajumbe walijadili na kukubaliana.

### **NENO TOKA KWA M/KITI WA CCM**

Mwenyekiti wa CCM aliwashukuru Wajumbe, na kuwaomba Waheshimiwa Madiwani kuendelea na kasi ya Mh. Rais wa awamu ya tano(5) wa Jamuhuri ya Muungano Tanzania Dkt. John Joseph Pombe Magufuli.

### **MUHTA NA 18/2015/2016: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote waliohudhuria kikao kwa namna ya pekee, kwa jinsi wajumbe walivyojadili agenda za kikao, yote yaliyojadiliwa ni kwa maslahi ya wananchi wa Ngara, katika kujadili taarifa lazima tufuate kanuni, aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kuweka ratiba ya kuwatebelea wananchi na yale maswali yatakayoulizwa na wananchi basi yajibiwe vizuri yale yatakayoshindikana kuyapatia majibu basi mawasiliano na Wataalam yafanyike, Alimuomba Mkurugenzi Idara zote wafanye ziara viji alishukuru uongozi wa CCM. Kikao kilifungwa saa 9.46 Alasiri.

**UMETHIBITISHWA**

.....

**Mh. Erick Nkilamachumu Bw. Kevin S. Makonda**

**MWENYEKITI**

**KATIBU**

**Tarehe...../.....2016**